POWERED BY
WWW.MANYAMFRANCHISE.COM

**Swali la 49**

Mwandishi wa taarifa hii ana msimamo kuwa:
A. ustaarabu wote wa kigeni unapotosha maadili
B. maadili yatafaulishwa na vijana na serikali husika
C. uigaji wa nyendo za kigeni unapaswa kuzuiwa
D. ujenzi wa ghorofa duni na njama za kifisadi zimezidi

**Matokeo ya swali la 49**

| Majibu | A | B* | C | D |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 28.56 | 20.31 | 33.42 | 16.31 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine | 27.20 | 28.71 | 28.25 | 24.37 |

* Inaonyesha jibu sawa

Swali hili lilitahini mbinu ya tathmini. Hapa pia, kama swali la ***48***, watahiniwa walikuwa wanakisia majibu. Mwandishi wa kifungu hakusema kuwa utamaduni wote wa kigeni ni mbaya kwa hivyo hawezi kusema uigaji wa nyendo za kigeni uzuiwe. Taarifa inazungumzia juu ya ufisadi kwa jumla kwa hivyo huo hauwezi kuwa msimamo wa mwandishi. Mwandishi yeyote akiandika lazima aonekane kutoa suluhisho ikiwa anaandika kuhusu tatizo fulani katika jamii – Naye huyu mwandishi hapa amejaribu kupendekeza suluhisho. Amezungumzia juu ya mikakati ya serikali kutafuta suluhisho na pia akataja kwamba vijana ndio wajenzi wa taifa wa leo na kesho. Kwa hivyo msimamo wake ni ***B. Maadili yatafaulishwa na vijana na serikali husika.***

## 4.2 SEHEMU YA PILI : INSHA

Mwaka wa 2007 insha ilikuwa

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu juu ya kichwa kifuatacho:

Rafiki yako amehamishwa na kujiunga na shule nyingine. Mwandikie barua ukimwelezea maendeleo yako tangu mlipoachana.

Insha hii ni ya kirafiki kwa hivyo haikuwa na mahitaji mengi kwa mtahiniwa. Mtahiniwa amepewa uwanja mpana wa kujieleza na kuandika insha yake kwa njia inayopendeza bora asitumie lugha kwa mfano isiyo ya adabu.

Yafuatayo ni maelezo ya kuonyesha jinsi alama katika viwango vine maalum zinavyofikiwa katika usahihishaji. Viwango hivi ni alama ***01-10, 11-20, 21-30, 31-40.***

### 4.2.1 Kundi la kwanza (alama 01-10)

Watahiniwa hawa, hasa wale waliotuzwa alama ***01-05***, huandika insha zao vibaya mno. Wao hutumia maneno ya Kiswahili,ya Kiingereza na lugha zao za mama yakichanganywa. Kuna baadhi wanaotumia lugha isiyoeleweka hata kidogo. Wale wanaotuzwa alama ***6-10*** huwa wameandika insha zao kwa Kiswahili kilicho na makosa mengi sana ya sarufi na tahajia. Pia mawazo yao hayatokei vizuri. Huwa pia wamepotoka kwa upande wa mada.

TEL: 0728 450 425

**Mtungo wa kwanza**

SHULE YA NTHONGONI,
P.O. BOX 51,
KIBWZE,
13-11-2007.

Shule ya moto kusakubauma ya nilukula na ukutan. Changa al Mabauct alilanlula kula ya huya ulaura. Chanzeanula zalant adauezat pia. Nilangaal kula Shule ya ulofo sanikulang ifarulany nilkulanshya.

Huyn Kaula na Mama alusantendeza Chang ya ulatulkya. Baaday an aluchang ganeli mbi Maameluy na Shule ya alurlan Shele ulanufuleany ya bauehafkulara. na Sana huyaueza haulaza parelia Mulandikanyi ya naling luyant zelulan za na heulanega.

Siku moja Shule an hijanantaula chankna alirulankula. ula hijezakuld machang harulta ulafemkulan. kula anehanukus Shele ya maah alikulang mmoja kula. Chaneuki hi an mabi Siku ifnakewa anehakulha ja Sana yekaws ya henotuulhag alinakulan na ulhauchira Mulansha. yatzolkeuet na ukuula anueha kula Shule kula mato yefaucakue ya ulfakra. Baaday Cnasuea ya ulakrijhi na Sana Pia Wa Maendakuula. Kuula alikarula Changua hii walanaulana.

Kula nilulanhuyn mulachaneg Cha yetzant hnyanzakula na Sana fanulareang ya Mlaka hikuu afikulang. hikulanl kula ulamang yote jankulakna

anikuthi ya Kuwa ilanutang kw Mohauankma na Sanfikusan. Ulafenye zeulan ya Mabauzanhi Kazeuanya alikuafizan an yefazuchi kula Sana Nlenaulha Nilaniwa hiantukula jhauh ula wafakna adikaulang na Sanifkusan ahallang kula Chaja Mulanikanifa ya Paula Machanzeli yote.

*(alama iliyotuzwa 02)*

Mtunzi wa insha hii hawasiliani na wala maneno aliyotumia hayaeleweki.

**Mtungo wa pili**

Linet odhiambo
shule ya msingi ya papa
S.L.P. 401163.
mombasa.

Elizabeth Ndinda
Shule ya msingi ya wangu
S.L.P 50516
Nairobi

Kwamba ni salamu mingi kutoka pahali niko huku Nairobi. Nadhani wewe ni mzima kama mimi vile nilivyo natumaini ya kwamba mola amekupa Raha sufusufu.

Ya kwanza ni kuwa ni kutoka uhamishwe hii shule yetu huku buruburu na ukajiunga na shule ya Shirandula huko mombasa ya kwamba tangu tulipoachana nimehendelea vizuri sana katika masomo yangu huku nikiomba mola niendelee vivyo hivyo. katika muhula wa kwanza nilikuwa na alama za juu huku nikiongoza shule yetu nambari moja.

Tangu ulipoenda mombasa roho yangu haina raha ya kwamba tamaa mbele mauti nyuma na hivyo ndivyo mambo yako huku Nairobi na kusifu na kuziiga ya kweli siki la kufa alisikii dawa. Niliketi peke yangu huku nikiwanza na kuwazua huku nikiwa na vitabu vyangu mikononi hata kulala siwezi nikikufikiria na tokwa na majozi hata sikuli.

Nataka mola akuongezee miaka mingi huendelee kufanya kama mimi

| | |
|---|---|
| Hesabu nilikuwa | 98% |
| Sayasi | 100% |
| somo la ziada | 78% |
| kiswahili | 88% |
| Kiingereza | 94% |

Zote zikiunganishwa nilikuwa na alama mia nne na sitini na saba (467) na taka pia mtihani ya kwenda kidato cha kwanza hufanye hivyo na huongezee zingine kama ishirini na huache pilkapilka zenye nimesikia huko kwenyu mombasa. Nashukiwa na nyota ya jaha.

Vyote vingaavyo si dhahabu chambilecho wahenga kwa hivyo tia bidii kwa masomo ndio kila kitu bila masomo huwezi pata kazi mzuri na hakuna mtu yeyote atandika adinasi kama achasoma.

Mwisho nataka kukujulisha ya kwamba soma na huache hii mamba ya kucheza na masoma dunia ni baya na kama husomi

hakuna kitu kingine hunaweza fanya isipokuwa kuiba vitu vya watu na hutakufa.

Kwa rafiki
mpendwa
Elizabeth Ndinda
SP.

*(alama iliyotuzwa 09)*

Mtahiniwa huyu amejaribu kuandika insha yake kufuata mada aliyopewa. Hata hivyo amepotoka sana kwa mtindo wa insha yake na sarufi yake ni mbaya. Amefanya makosa mengi sana ya hijai.

**Kundi la pili (Alama 11-20)**

Kundi hili ni la wale wanaoonyesha kuimudu lugha kidogo na wanaweza kuandika sentensi na zikaleta maana. Wale waliotuzwa alama *16 -20* ni wale wenye mawazo yanayoweza kutiririka kidogo. Hata hivyo, wale wa alama *11-14* huwa hawapangi hoja zao vizuri, wanafanya makosa mengi ya sarufi, msamiati na tahajia, Wale waliotuzwa alama *15-20* huwa pengine wameandika hoja chache katika insha zao na hawakutumia lugha tamu ya tamathali. Insha zao huwa fupi pia.

**Mtungo wa tatu**

Kathure Eunice,
S.L.P. 200
Nanyuki,
14/11/2007.

Rafiki mpedwa
CAROLINE

Kwanza ni salamu zitokazo kwangu. Ninajua huko salama salimini huko shuleni Mbokwiko na ninajua kuwa unaendelea vizuri.

Ninaishukuru nafasi hii ili nikuulize jinsi unavyo endelea huko Mwamshukufu mungu kwa kunipa nafasi hii. Kutoka tulipoachana hakuna aliyemwandikia mwingine barua lakini naishukuru nafasi hii ili nikuandikie jinsi ninavyo endelea huku ambavyo tangu tuachane nanaendelea vizuri katika masomo yangu tulipoachana mimi niitia bidii katika masomo yangu na kutoka mwaka huo nimimi niikuwa nikianza katika darasa langu hakuna aliyekuwa akinishinda kwakuwa waliosema waliosema ukitaka cha mvunguni lazima uiiname, nilikuwa napewa zawadi kila tanapo fanya mtihani. Nataka kukujulisha kuwa ikuwa ulikuwa unaursoma vitabu vya methali na vingine vitabu vingine ulafuu kwakuwa asiyejua ngeu ngui kiswahili na ikuwa unajua izo rafiki yangu ninakuomba nakutakia baraka zito kazo kwa mwenyezi mungu kwakuwa mungu si adhumani hata kujaua.

Niku tu katika hali hii yakukujulisha ingawa uko katika shule hii tu tugekuwa tunasoma mei hii pamoja, mwalimu mkuu ana kukumbuka anapoingia katika darasa kutufundisha endelea na mtihani wako vizuri tunaonana tuendapo nyumbani.

Shule inaendelea vizuri kabisa kuijengwa vizuri hata utakapo kuja nitakupeleka kwa sababu uweze kwenda wewe peke yako utaniandikia unambie utakapo kuja nikupeleke siku hiyo utakapo nikupeleke hautadhani ndio shule uliokuwa unadhani hiyo shule ya upili iliyokuwa kanbu na yetu kwa vile ilijengwa upya hata duniya kwa mbeleni siyo tunaongezeka tukawa wengi, ulipo enda mimi sikupata mwingine kama wewe kwakuwa wewe na mimi tulikuwa marafiki wa kufana kusikana niwewe tu na kutakia baraka kumbuka ili tuende shule ya upili pamoja.

Mimi wako mwaminifu

Kathure [illegible],

(Alama iliyotuzwa 11)

Mwandishi ameandika insha yake kufuata mada aliyopewa lakini amefanya makosa mengi sana ya sarufi na hijai. Aya zake zinaingiliana na haijulikani sentensi zake zinaishia wapi.

*Mtungo wa nne*

Shule ya Msingi ya Kiandungu,
S.L.P 182,
Igoji Meru.
Tarehe 14/11/2007

Kwa mpendwa Mukami

Habari yako rafiki? nadhani ni nzuri. pia yangu ni nzuri kutoka wakati tulipoachana.

Ninachukua fursa hii kukuandikia barua hii nikujulishe vile ninavyoendelea. Hapa ~~niko~~ shuleni niko salama salimini. Nimeendelea sana hapa shuleni kwa sababu kutoka wakati ulipohama niliazana kuwa nambari ya kwanza na hata nikaongeza makisi nyingi sana. Sasa mwalimu wangu ameniambia kuwa atanipea zawadi tele.

Nyumbani wazazi wangu wanafuraha riboribo kwa vile nimefanya. Wazazi wamenizumsha kuwa wana zawadi nyingi zangu. Wakati ulipoenda tulianza kusoma kwa bidii za mchwa kwa sababu hata hao wengine wametia bidii.

Shuleni yetu nimechaguliwa kuwa kiralo wa darasa kwa vile walimu wameona nikitia bidii sana. Ulipoenda mwalimu mkuu aliwaita wazazi shuleni ili tuweze kupewa zawadi. Nilikuwa na furaha mpwitampwito kwa sababu mtihani tuliaufanya nilikuwa nambari ya kwanza.

Wazazi walipoingia shuleni tuliwakaribisha kwa makofi. Mwalimu mkuu alipiga kengele na sote tukakusanyika. Aliwakaribisha wazazi tena na tukaanza kupewa zawadi. Nilikuwa na furaha tele kwa sababu nilikuwa wa kwanza kuitwa. Nilipojitokeza nikiwa ninajisinga kama tausi. Mwalimu mkuu alinipongeza kwa vile nilikuwa

nimefanya. Alinipatia zawadi tele na nikarudi nikiwa na furaha.

Kutoka siku hiyo mwalimu mkuu alisema ni mimi kiranja wa shule yote. Wanafunzi wenzangu waliposikia hivyo walishangilia sana. Hata sasa ni mimi kiranja wa shule yetu. Wazazi wangu hata wao waliniandalia sherehe kubwa sana. Nilipewa zawadi nyingi hata siwezi hesabu. Mjomba wangu naye aliniletea vitabu vya kusoma na nina hakika ninaendelea vizuri sana. Nimeendelea sana na hata wewe nadhani unaendelea.

Kwa aila yetu hakuna mwingine mwerevu huliko mimi. Wazazi wangu wananipongeza kwa vile nimefanya. Wasalimie wazazi na watoto wenu wote.

Ni mimi wako

Kinanu mwenia

*(Alama iliyotuwa 20)*

Mtahiniwa huyu ameanza insha yake vizuri. Amepanga kazi yake katika aya na hati yake ni nzuri.Hata hivyo, insha yake ni kavu na haina utamu wa tamathali na msamiati unaovutia. Ametoa hoja moja tu ya mandhari ya shuleni. Amefanya makosa mengi ya sarufi na insha yake ni fupi.

**Kundi la tatu (alama 21 – 30)**

Hawa ni wale ambao wameshughulikia maudhui ya insha. Wengi hupoteza alama kwa kutumia lugha isiyokolezwa semi ama pengine wakatumia semi visivyo. Makosa ya kisarufi, tahajia na msamiati pia huwakosesha alama. Urefu usioridhisha wa insha zao huweza kuathiri alama kwa sababu huenda hoja zisikamilike, au kutosha kihoja.

**Mtungo wa tano**

Shule ya msingi ya mkumu.
S. L. P 1045.
KAKAMEGA.
14-11-2007.

kwa rafiki mpendwa Corazon Soita

Pokea salamu nyingi kutoka kwangu, natumai u mzima kama kisiki cha mkalitusi huku pia mimi nikiwa mzima kama kigogo.

Ningependa kuandika hii barua kukuelezea ninavyo endelea tangu tulipoachana na wewe na ukaenda kujiunga na shule ya msingi ya mkumu huko kakamega. Mimi hapa ninaendelea vizuri sana tukiwa na familia yetu hapa Nairobi hata wamekusalimia sana.

Natumahi pia wewe mahali ulipo unatukumbuka na tunazidi kuombeana kila lakheri kwa masomo yetu hata maisha yetu. Kwa masomo yangu mimi nilikuwa naendelea vizuri tulipoachana nikiwa darasa la sita na nilikuwa nafuzu vizuri hata tulikuwa tunafanya mtihani nina kuwa wa kwanza darasani walimu wana furahia sana nilikuwa mwanafunzi wa heshima sana shuleni na nilikuwa na mudu usafi Walimu wa shule yetu wakanipenda sana kwa heshima yangu na kunipongeza sana hata nilipomaliza darasa la sita na kwenda la saba niliweza

kufurahia sana sikuweza kurudi nyuma hata dakika moja wala kupoteza wakati wangu kwa marafiki wabaya niliweza kwenda na werevu wangu, hata watu wakaweza kunipenda zaida hata nilikuwa nasaidia wanafunzi wa darasa letu ambao hawa kuwa wanajua somo la hesabu kwa sababu hilo ndilo somo ambalo nilikuwa na lipenda zaidi kuliko somo zingine.

na nilikuwa napita vizuri Kisha na tunukiwa zawadi maarufu Sana.

Hata Sasa niko darasa la nane nakalia mtihani wangu wa kimataifa (K.C.P.E) na nina matumaini kuwa nitapita mtihani huu kwa alama mia nne kuendelea. Nikimalizia ningependa kukuambia ya kwamba tukumbukane kwa maombi kila wakati na uweze kufaulu mtihani wako.

mimi wako mwaminifu,

ELIZABETH MUSIMBI

(Alama iliyotuzwa 22)

Mtahiniwa huyu amekosa alama nyingi kwa kutumia lugha kavu isiyokolezwa semi na tamathali. Amefanya makosa mengi ya kisarufi kama vile kuandika herufi ndogo badala ya kubwa, kutoakifisha kazi yake na pia makosa mengi ya tahajia.

Baadhi ya makosa ni:

*Nina kuwa*
*Na lipenda*
*nairobi*
*ninavyo endelea*

**Mtungo wa Sita**

JOYCE ACHIENG
SHULE YA MSINGI UHURU
SLP 1187,
BURUBURU.
NAIROBI.
14|11|2007.

Rafiki mpendwa Pamela,

Habari yako? Natumai ya kwamba uko sawa na pia u mzima mithili ya

Kigongo. Mimi niko salama salimini na ninaendelea vizuri na masomo yangu.

Mathumuni ya kuandika hili waraka ni kwasababu nataka kukujulia hali na nikueleza ninavyoendelea na maisha huku shuleni baada ya kuhamia kwako chambilecho wahenga "barua ni nusu ya kuonana."

Kama nilivyokueleza awali, nataka kukufahamisha ninavyoendelea shuleni kinagaubaga.

Jambo la kwanza ambalo ningependa ujue ni kwamba tumeletewa mwalimu mgeni baada ya Bw Otieno kustaafu. Mwalimu huyu anajulikana kama Bw Macharia. Yeye ni mwalimu mpole na mwenye heshima. Waama wahenga, heshima si utumwa. Ni mweusi tititi mithili ya makaa. Ni mcheshi na punde tu anapocheka utapata nafasi ya kuziona meno zake ambazo ni nyeupe pepepe, theluji kando.

Jambo la pili, niko na furaha isiyo na kifani kwa sababu mimi ndiye kiranja mkuu wa shule baada ya walimu kuona tabia zangu njema. Wahenga na wahenguzi hawakutuchana nywele kwa mfupa wa ngisi waliponadi ya kwamba chema chajiuza, kibaya chajitembeza. Isitoshe mcheza kwao hutuzwa.

Jambo la tatu ni ya kwamba shule yetu imepakwa rangi upya. Tulikuwa tumezoea kuta chafu lakini sasa shule yetu inamerementa metumetu nyota kando.

Wahenga hawakutuvalisha soksi za glasi walipo nadi. "Pasipobudi hubidi" Wanafunzi wa darasa la nane hawana budi kutoka shuleni sa moja jioni, kwani wao hubaki shuleni kwa minajili ya kufanya masomo ya ziada.

Sina budu kumalizia kwa kusema ya kwamba tunajitahidi sana katika masomo yetu. Chambilecho wahenga "Mvumilivu hula mbivu".

Natumai nawe pia utaniandikia barua hivi karibuni.

Nisalimie wavyele wako na pia dada yako.

Ni mimi wako
Joyce.

*(Alama iliyotuzwa 29)*

Insha hii imeandikwa vizuri. Mwandishi amejieleza vizuri na kupanga kazi yake vizuri katika aya. Hata hivyo, amefanya makosa ya sarufi na hijai kama:

| | | |
|---|---|---|
| *kwasababu* | - | *kwa sababu* |
| *hili waraka* | - | *huu waraka* |
| *meno zake* | - | *meno yake* |
| *meno ambazo* | - | *meno ambayo* |
| *sa* | - | *saa* |
| *budu* | - | *budi* |

Baadhi ya aya zake ni fupi sana.

**Kundi la nne (alama 31- 40)**

Hawa ni wale mabingwa kweli katika uandishi wa insha. Wanaimudu lugha vizuri na wanashughulikia maudhui vilivyo. Insha zao zinavutia kwa hati safi, aya zilizopangwa vizuri, msamiati unaokubalika na wingi wa tamathali za usemi.

Wale waliotuzwa alama *36* hadi *40* huwa wameandika insha za kipekee na za kiwango cha juu zaidi. Katika kiwango hiki makosa ya aina yoyote ile ni nadra kupatikana. Insha hizi huwa za urefu unaoridhisha.

**Mtungo wa saba**

Eunice Kadzo,
Shule ya msingi ya kahawa,
S. L. P 10479,
Nairobi,
4 NOV, 2007.

Kwa sahibu mpendwa Rodha,

Natumai uko buheri wa afya na mzima kama kigongo. Hapa Nairobi wavyele wangu pamoja na ndugu zangu wako salama na wanaendelea vizuri. Tangu tulipoachana na wewe nimekuwa nikiendelea vizuri na masomo yangu. Nilipelekwa katika shule nyingine ambayo ni nzuri zaidi kuliko ile ya kwanza. Najikaza kisabuni na kutia bidii masomoni kama mchwa ili mwishowe nivune nachopanda na kama ujuavyo mtu huvuna anachopanda nami bila shaka nitavuna mazuri

Mimi huamka asubuhi na mapema kabla jimbi hajawika na kuanza masomo yangu. Sifanyi mchezo ambao nilikuwa nafanya hapo awali kwa maana, niligundua kuwa duniani huwezi kufanikiwa bila kutoa jasho lako mwenyewe kama walivyosema akina babu zetu kuwa mtegemea cha nduguye hufa maskini nami sitaki kufa maskini hohe hahe

Baba alininunulia vitu vingi vya kuchezea na isitoshe alinunua tarakilishi ambayo mimi hutumia

kama ninasoma.Nilijiunga na klabu cha vijana ambacho huwasaidia watu ambao hawajiwezi na pia walioathiriwa na ugonjwa hatari wa ukimwi.Kila juma sisi huwatembelea na kuwahimiza jinsi ya kuishi na ugonjwa huu.

Wakati mwingi, mimi huendo maktabani na kupitia vitabu kadha wa kadha kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame na wala sio kusimama wima kama askari jela.Nilijaribu kuwatafuta marafiki wengi wa kukaa nao na nilifanikiwa kumpata mmoja tu!Lakini wewe ndiye rafiki yangu wa chanda na pete kufa kuzikana na isitoshe wazazi wetu wanaishi karibu kama pua na mdomo.

Uk mzinga wa nyuki umeendelea na una nyuki wengi na wao hutengenezo asali ambayo mimi huuza na kupata ngwenje za kutumia kwa kununulia vitu vyangu mbali mbali.Nilikuwa na furaha mithili ya tasa aliyeweza kujifungua mapacha mwezi uliopito kwa kuibuka mshindi katika mashindano ya kuiba mashairi Nilikuwa mwanafunzi bora zaidi katika mkoa wetu.

Mimi kama mmoja wa vijana nilijiunga na marafiki wenzangu kupinga utumizi wa mihadarati na ngono kabla ya kufunga ndoa.Tuliandamana pamoja na mabango njiani kwa juma moja.Vijana wengi walijitokeza na kuunga mkono na pia chifu wetu alitupa mkono wa tahania kwa kazi nzuri.Sina mengi ya kusema bali nikukuhimiza ulie bidii masomo. Natuma tutaonana hivi karibuni shule zikifungwa na pia uwape wazazi wako mkono wa buriani pamoja na nduguzo.

Rafikiyo wa chanda na pete

Eunice kadzo.

Rodha Rehema,
S.L.P 0079.
Kampala.

*(Alama iliyotuzwa 31)*

Insha hii inavutia kwa tamathali za semi, hati safi na kupangwa katika aya. Mwandishi amejaribu kutoka katika mazingira ya shule kuelezea mambo mengine lakini hakukuza hoja zake vizuri, hali ambayo imemkosesha alama za juu zaidi ya alizotuzwa. Amefanya makosa machache ya tahajia na ya sarufi.

Mifano:

| | | |
|---|---|---|
| natuma | - | natumaini |
| kuiba mashairi | - | kuimba mashairi |

ukimwi badala ya UKIMWI

**Mtungo wa nane**

Allan Kuria,
S.L.P. 21784-00505,
NAIROBI
Novemba 14, 2007.

Kwa mwandani Msanifu,

Nakumiminia salamu bwaibwai mfano wa thureya za nyota tupilia mbali wana wa Ibrahimu. U rai gani? Ni rajua yangu kuwa una siha njema na u mzima mfano wa ngarange ya mpingo.

Madhumuni na dhamira kuu ya kukuandikia waraka huu si kukusabahi,

mbali ni kukueleza kwa mapana na marefu maendeleo yangu hapa shuleni. Tangia ulipojiunga na Shule ya Matopeni, hapa Chongoleani pamekuwa na maendeleo tumbi nzima.

Kwanza, tuliachana nikiwa karibu kuburura mgwisho darasani. Sasa, nina furaha isiyo mfanowe kukujulisha kuwa sasa, matokeo yangu ni aula zaidi. Katika mtihani uliopita, niliuma uzi na kukwangura maksi gana nne wahedi wa sabini. Mwanagenzi mmoja tu ndiye aliyenipiku, naye aliibuka namba moja kwa alama mia arba sabini na mbili. Kwenye mtihani unaokuja, nimepania kumpiku na maksi si kidigi.

Pia, kuna wafunzi wageni ambao wameajiriwa shuleni mwetu. Wadarisi hawa wameletwa ili kutufunza badala ya walimu walioenda njia ya marahaba kwenye ajali ya barabarani. Ingawa walimu hawa ni wapya shuleni kwetu, si wageni asilani kwenye uwanja wa ufunzi.

Bwana Kokotoo, ambaye ni mdarisi wa Hisabati, ni mwalimu mufti kabisa. Yeye hupenda nambari mithili ya mboni ya jicho lake. Kufeli kwenye Hisabati ni sawa na kujitukana mwenyewe. Bi Safuni naye ni bingwa kwenye lugha

ya mayai. Yeye hukitongoa na kukisongoa Kimombo kana kwamba alizaliwa Uingereza. Siku hizi, sisi hustihizai mitihani ya Kiingereza. Ustadh Obonyo naye ni galacha kama si ulama katika Kiswahili Ustadh hukitema Kiswahili kama aliyekopola na kamusi mkononi. Yaumu hizi, kupasi Kiswahili ni rabisi kama mboga.

Kwenye kitengo cha upishi, ukarabati pia umefanywa. Wapishi wazee waliokuwepo wamepigwa kalamu na wengine wageni wakapewa ajira. Wapishi hawa wana tajiriba chungu nzima. Wao hutuandalia maakuli ya kunoga na kuhomolewa. Wengi hutoka humo wakiramba vyanda na viganja vya mikono yao kweli, aisifuye mvua imemnyea.

Isitoshe, bwawa lililokuwa likiakwa limekamilika. Bwawa hili lilikuwa limechukua miaka minne kujengwa kikamilifu, lakini wazee wa konga za mawe hawakuwa na ubozi wa kaa walipomadi, kawia ufike. Sasa, tunajua samaki ni nani na limbukeni ni kina nani kwa hisani ya bwawa hilo.

Kwa vile wasaa umenipiga kumbo, sina budi kutia kitone cha mwisho,

kwani lisilo budi hubidi na likibidi hutendwa. Nitakuwa mwingi wa furaha tamthili ya hawinde aliyeokota vipande vya almasi ya Mwadui nitakapoisoma risala yako. Mbali na hayo, usighafilike kuwasabahi ndugu zako Nana na Vumilia na wahebi wangu, kina Kitwana na Rashid. Wajuvye kuwa bado sijawazika kwenye mava ya mghafala.

Mimi wako wa jua na mvua,

~~Allan~~

Allan Kuria.

*(Alama iliyotuzwa 38)*

Insha hii imeandikwa kwa ufundi mkubwa. Kazi imepangwa vizuri kwa sentensi na aya na hati inayovutia. Urefu wake unaridhisha kabisa. Makosa ya aina yoyote ni machache sana. Mtahiniwa amejaribu kueleza mambo tofauti tofauti katika mazingira ya shule. Amefanya kosa la tahajia.
wafunzi - wakufunzi ·

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

4.3.1 Ni vizuri mfundishe Kiswahili katika ujumla wake. Tafuteni vitabu ambavyo vimependekezwa na kuvitumia kufundishia.

4.3.2 Sisitizieni wanafunzi kuwa wakijibu maswali ya vifungu ni lazima wasome kifungu chote ili waweze kujibu maswali, wala wasijikite tu pale wanapofikiria kuwa swali limetoka.

4.3.3 Fundisheni kuwa maswali ya kifungu cha ufahamu ambayo hayaonekani kuwa na majibu moja kwa moja huulizwa katika mtihani. Wasaidieni kuzoea kujibu maswali ya aina hii. Maswali haya huweza kuwa ya stadi kama ya tathmini ambayo ni stadi ya juu katika zile stadi za ***ujuzi, ufahamu, matumizi, uchanganuzi, usanisi*** na ***tathmini.***

4.3.4 Wanafunzi wenu ni lazima wasome kichwa cha insha na kuelewa mada na kutoa hoja nyingi. Si vizuri kutumia msamiati mkubwa ama mwingi mwingi ambao unapoteza maana iliyokusudiwa ama kutumika vibaya tu.